ASb approved

Hadithi kumhusu Wangari Maathai

Ursula Nafula

Maya Marshak

Kiswahili

African Storybook.org

Msichana mdogo alifanya kazi shambani na mamake. Waliishi karibu na Mlima Kenya, Afrika Masariki.

Msichana huyo aliitwa Wangari.

Wangari alilima katika bustani ya familia yake. Alipanda mbegu ndogo katika ardhi yenye joto.

Alipenda majira ya jioni, wakati jua lilipotua. Giza lilipozidi, Wangari alienda nyumbani.

Wangari alikuwa mwerevu. Alikuwa na hamu ya kwenda shule. Lakini, wazazi wake walitaka awasaidie nyumbani. Alipofikisha umri wa miaka saba, alianza kwenda shule.



Wangari alipenda kusoma.
Alijifunza kupitia kila
kitabu alichosoma.
Alifanya vyema shuleni.
Alialikwa kwenda Amerika
kuendeleza masoma yake.

Wangari alichangamshwa
sana na nafasi hii.
Alipenda kuujua
ulimwengu zaidi.



Alipokuwa chuoni huko Amerika, Wangari alijifunza mambo mapya. Alisomea mimea na jinsi inavyokua.

Alikumbuka vile alicheza na ndugu zake. Alikumbuka kivuli cha miti maridadi ya misitu ya Kenya.

Alipojifunza, alifahamu kuwa aliwapenda watu wa Kenya. Alitaka wafurahi na wawe huru. Alikumbuka kwao nyumbani Afrika.

Wangari alikamilisha masomo yake akarudi Kenya. Nchi yake ilikuwa imebadilika sana.

Matajiri walikuwa wameikata miti. Wanawake walikosa kuni. Watu wengi walikuwa maskini. Watoto walikuwa na njaa.

Wangari aliwafunza wanawake kupanda miti. Waliiuza miti hiyo na kupata pesa. Walizitumia kwa mahitaji ya familia zao. Walifurahi kwa sababu Wangari aliwasaidia kuwa na nguvu na uwezo.



Muda ulipopita, miti mipya ilikuwa misitu. Mito ilianza tena kupitisha maji. Ujumbe wa Wangari ulienea Afrika nzima.

Leo, mamilioni ya miti imemea kutokana na juhudi za Wangari.

Wangari alikuwa amefanya bidii. Watu ulimwengu mzima walifahamu hili. Walimpa Tuzo la Amani la Nobel.

Wangari alikuwa mwanamke wa kwanza wa Kiafrika kupokea tuzo hilo.

Wangari aliaga dunia mwaka 2011. Tunaweza kumfikiria kila tunapouona mti wa kupendeza.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Hadithi kumhusu Wangari Maathai

Author - Nicola Rijsdijk
Translation - Ursula Nafula
Illustration - Maya Marshak
Language - Kiswahili
Level - First paragraphs

© Nicola Rijsdijk, Maya Marshak, Tarryn-Anne Anderson, Bookdash.org and African Storybook Initiative, 2015
Creative Commons: Attribution 4.0
Source www.africanstorybook.org